# WIZARA YA AFYA

## HOSPITALI YA RUFAA KANDA YA KUSINI - MTWARA

## TANGAZO LA AJIRA YA KUJITOLEA

Uongozi wa Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini – Mtwara, kwa niaba ya Katibu Mkuu Wizara ya Afya, inatangaza nafasi **51** za Ajira ya kujitolea kwa kipindi cha mwaka mmoja (1) kama ifuatavyo: -

**1.0 Daktari Daraja la II – (NAFASI 05)**
**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini
**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

**1.1 SIFA**

Kuajiriwa wenye Shahada ya Udaktari kutoka Vyuo Vikuu/Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali waliomaliza mafunzo ya kazi “Internship” ya muda usiopungua miezi kumi na miwili na kupata usajili kutoka Baraza la Madaktari Tanganyika (Medical Council of Tanganyika).

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Daktari |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | ▪ Kufanya kazi zote za matibabu hospitalini zinazohusiana na magonjwa mbalimbali yakiwemo magonjwa ya watoto, magonjwa ya akina mama na upasuaji wa kawaida na wa dharura.<br>▪ Kutoa na kusimamia elimu ya afya pamoja na kuboresha afya ya jamii katika Wilaya na Mikoa au eneo lake la kazi.<br>▪ Kuchunguza, kufuatilia na kuzuia milipuko ya magonjwa.<br>▪ Kufundisha wanafunzi na watumishi waliopo kwenye eneo la kazi. |

| | |
|---|---|
| | ▪ Kusimamia na kuelekeza wafanyakazi walio chini yake.<br>▪ Kubuni na kuendesha utafiti na kusambaza matokeo.<br>▪ Kubuni na kutayarisha mikakati ya kuinua ubora wa huduma ya fani yake.<br>▪ Kushiriki, kuhakiki na kuboresha huduma za afya (medical audit and quality improvement).<br>▪ Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake. |

### 1.3 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la Mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 2.0 Afisa Muuguzi Daraja la II – (NAFASI 05)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini
**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 2.1 SIFA

Kuajiriwa wenye Shahada (Degree) ya Uuguzi na Ukunga, waliomaliza mafunzo ya kazi "Internship" ya muda usiopungua miezi kumi na miwili na kupata usajili kutoka Baraza la Uuguzi na Ukunga Tanzania (Tanzania Nurses and Midwifery Council).

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Afisa Muuguzi Daraja II |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | a) Kutoa huduma za uuguzi<br>b) Kukusanya takwimu muhimu za afya.<br>c) Kuwasimamia na kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake<br>d) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya<br>e) Kufanya utafiti na ubunifu ili kuboresha huduma.<br>f) Kutoa huduma za kinga na uzazi<br>g) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake |

### 2.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 3.0 Afisa Muuguzi Msaidizi Daraja la II – (NAFASI 10)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini

**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 3.1 SIFA

Kuajiriwa wenye Stashahada (Diploma) ya Uuguzi, ya muda usiopungua miaka mitatu kutoka Chuo kinachotambuliwa na Serikali, waliosajiliwa na Baraza la Wauguzi na Wakunga Tanzania (Tanzania Nurses and Midwifery Council).

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Afisa Muuguzi Msaidizi |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | a) Kutoa huduma za uuguzi<br>b) Kukusanya takwimu muhimu za afya.<br>c) Kuwaelekeza kazi wauguzi walio chini yake<br>d) Kuelimisha wagonjwa na jamii kuhusu matatizo yao ya kiafya<br>e) Kutoa huduma za kinga na uzazi<br>f) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkuu wake wa kazi zinazohusiana na elimu, uzoefu na ujuzi wake |

### 3.3 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 4.1 Fundi Sanifu Umeme Daraja la II - (NAFASI 01)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini

**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 4.2 SIFA

Kuajiriwa mwenye cheti cha kidato cha nne na cheti cha ufundi Sanifu Umeme kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Fundi Sanifu Umeme |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | a) Kufanya kazi zote za fani ya umeme kwenye majengo yote ya Taasisi<br>b) Kufanya kazi ya kutengeneza vifaa vya umeme.<br>c) Kufanya usanifu miradi midogo ya umeme, kusimamia jinsi ya kufunga mashine mpya za umeme zinazowekwa kwenye majengo yote ya Taasisi.<br>d) Na majukumu mengine atakayopangiwa na Mkuu wake wa kazi. |

### 4.3 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 5.0 Fundi Sanifu Bomba Daraja la II - (NAFASI 01)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini

**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 5.1 SIFA

Kuajiriwa mwenye cheti cha kidato cha nne na cheti cha ufundi sanifu Bomba kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Fundi Sanifu Bomba |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | a) Kufanya kazi zote za fani ya bomba kwenye majengo yote ya Hospitali<br>b) Kufanya kazi ya kutengeneza vifaa vya bomba.<br>c) Kufanya usanifu miradi midogo ya maji pamoja na kuzibua mifumo ya maji taka.<br>d) Na majukumu mengine atakayopangiwa na Mkuu wake wa kazi. |

### 5.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 6.0 Msaidizi wa chumba cha Kuhifadhia Maiti - (NAFASI 02)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini
**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 6.1 SIFA

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne waliopata mafunzo ya Afya katika fani ya afya na utunzaji wa maiti.

.

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Msaidizi wa chumba cha kuhifadhia Maiti |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | a) Kufanya usafi wa chumba cha kuhifadhia maiti<br>b) Kupokea, kuosha na kutunza maiti.<br>c) Kusaidia kufanya uchunguzi wa maiti.<br>d) Kazi nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi. |

### 6.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 7.0 Msaidizi wa Afya – (NAFASI 05)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini
**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 7.1 SIFA

Kuajiriwa wahitimu wa kidato cha nne wenye uzoefu wa kazi za kuhudumu kwa muda usiopungua miaka miwili katika mojawapo ya fani za Afya.

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Msaidizi wa Afya/Kufua Nguo za Wagonjwa |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | a) Kufanya usafi wa vifaa vya kazi, usafi wa wodi na mazingira<br>b) Kusaidia wagonjwa wenye ulemavu na wasiojiweza.<br>c) Kuchukua nguo za mgonjwa/wagonjwa na kuzipeleka kufuliwa.<br>d) Kuchukua sampuli za mgonjwa kwa ajili ya vipimo vya maabara na kufuatilia majibu.<br>e) Kumsaidia kumlisha mgonjwa asiyejiweza<br>f) Kazi nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi. |

### 7.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 8.0 Afisa Tehama Daraja la II - (NAFASI 01)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini
**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 8.1 SIFA

Kuajiriwa mwenye Shahada ya masomo ya kompyuta katika moja ya fani zifuatazo; Uhandisi wa Kompyuta/ Mitandao/ Mawasiliano na Elektroniki au Matengenezo ya Mifumo ya TEHAMA kutoka kwenye Taasisi/Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali.

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Afisa Tehama |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |

| KAZI NA MAJUKUMU | 1. **Sehemu ya miundombinu (Hardware and Networks):**<br>a) Kufanya ukaguzi wa ubora wa vifaa vya TEHAMA na kurekebisha ipasavyo.<br>b) Kufanya matengenezo TEHAMA, madogo madogo ya vifaa.<br>c) Kufanya matengenezo ya miundombinu ya TEHAMA.<br>d) Kukagua na kutambua vifaa vinavyohitaji matengenezo.<br><br>2. **Sehemu ya Mifumo ya Habari (Information Systems);**<br>a) Kufanya ukaguzi wa ubora wa programu- tumizi na mifumo ya habari,<br>b) Kufanya marekebisho madogo madogo katika program - tumizi,<br>c) Kuchukua hatua za kiusalama kulinda program - tumizi na mifumo ya habari,<br>d) Kutoa huduma kwa watumiaji wa program - tumizi na mifumo ya habari<br>e) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi zinazoendana na sifa na fani yake. |
|---|---|
| | |

### 8.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

### 9.0 Afisa Tehama Msaidizi Daraja la II - (NAFASI 02)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini
**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 9.1 SIFA

Kuajiriwa wenye Stashahada ya masomo ya Kompyuta katika moja ya fani zifuatazo; Uhandisi wa Kompyuta/ Mitandao/ Mawasiliano na Elektroniki au Matengenezo ya Mifumo ya TEHAMA kutoka kwenye Taasisi/Vyuo vinavyotambuliwa na Serikali

| **KAZI** | Afisa Tehama Msaidizi |
| --- | --- |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | 1. **Sehemu ya miundombinu (Hardware and Networks):**<br>a) Kufanya ukaguzi wa ubora wa vifaa vya TEHAMA na kurekebisha ipasavyo.<br>b) Kufanya matengenezo TEHAMA, madogo madogo ya vifaa.<br>c) Kufanya matengenezo ya miundombinu ya TEHAMA.<br>d) Kuchukua hatua za kiusalama kulinda vifaa vya TEHAMA.<br>e) Kukagua na kutambua vifaa vinavyohitaji matengenezo.<br>f) Kutoa huduma kwa watumiaji wa vifaa vya TEHAMA, Kusimamia ukaguzi na ufungaji wa vifaa vipya vya TEHAMA.<br>g) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na mkubwa wake wa kazi zinazoendana na sifa na fani yake.<br><br>2. **Sehemu Mifumo ya Habari (Information Systems);**<br>a) Kufanya ukaguzi wa ubora wa programu- tumizi na mifumo ya Habari.<br>b) Kufanya marekebisho madogo madogo katika program – tumizi.<br>c) Kuchukua hatua za kiusalama kulinda program - tumizi na mifumo ya Habari.<br>d) Kutoa huduma kwa watumiaji wa program - tumizi na mifumo ya Habari.<br>e) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi zinazoendana na sifa na fani yake. |

### 9.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 10.0 Afisa Habari Daraja la II - (NAFASI 01)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini
**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 10.1 SIFA

Kuajiriwa mwenye Shahada ya Uandishi wa Habari au sifa inayolingana nayo kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Afisa Habari |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | a) Kukusanya na kuandika Habari.<br>b) Kupiga picha.<br>c) Kuandaa picha za maonyesho.<br>d) Kuandaa majarida na mabango (Poster).<br>e) Kuandaa vijarida na Vipeperushi.<br>f) Kufanya kazi nyingine atakazopangiwa na kiongozi wake wa kazi zinazoendana na sifa na fani yake. |

### 10.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 11.0 Afisa Hesabu Daraja la II - (NAFASI 01)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini
**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 11.1 SIFA

Kuajiriwa wenye elimu ya kidato cha nne au sita na Shahada ya Uhasibu kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Kuandaa taarifa za hesabu |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |

| | |
|---|---|
| **KAZI NA MAJUKUMU** | a) Kufanya kazi zote za zinazohusu malipo mbalimbali.<br>b) Kushiriki kuandika taarifa ya mapato na matumizi.<br>c) Kushiriki kuandaa taarifa za maduhuli.<br>d) Kushiriki kufanya usuluhisho wa hesabu za benki na nyingine zinazo husiana na maswala ya fedha<br>e) Kuandaa taarifa mbalimbali za mishahara.<br>f) Kufanya kazi nyingine za fani yake atakazo pangiwa na mkuu wake wa kazi. |

### 1.1 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 12.0 Afisa Masoko Daraja la II - (NAFASI 01)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini

**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 12.1 SIFA

Kuajiriwa mwenye cheti cha kidato cha nne au cha sita na Shahada ya masomo ya huduma kwa wateja kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Afisa Masoko |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | Kuwapokea wateja na kuwaelekeza maeneo ya kupata huduma.<br>Kupokea maoni na changamoto za wateja.<br>▪ Kushauri uongozi namna bora ya kuboresha huduma kwa wateja.<br>▪ Kuitangaza Taasisi kwenye vyombo/maeneo mbalimbali.<br>▪ Na majukumu mengine atakayopangiwa na Mkuu wake wa kazi. |

### 12.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

### 13.0 Msaidizi wa Kumbukumbu Daraja la II - (NAFASI 10)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini
**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

#### 13.1 SIFA

Kuajiriwa wenye elimu ya kidato cha nne au cha sita na stashahada ya kawaida katika fani ya utunzaji wa kumbukumbu katika mojawapo wa fani za afya, masijala, mahakama na ardhi.

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Msaidizi wa Kumbukumbu |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | ▪ Kutafuta kumbukumbu /nyaraka/mafaili yanayohitajiwa na wasomaji.<br>▪ Kudhibiti upokeaji, uandikaji wa kumbukumbu na nyaraka.<br>▪ Kuchambua, kuorodhesha na kupanga kumbukumbu na nyaraka katika reki, masijala /vyumba vya kuhifadhia kumbukumbu.<br>▪ Kuweka kumbukumbu (barua, nyaraka n.k) katika mafaili.<br>▪ Na majukumu mengine atakayopangiwa na Mkuu wake wa kazi. |

#### 13.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

### 14.0 Afisa Ustawi Msaidizi II - (NAFASI 01)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini
**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

#### 14.1 SIFA

Kuajiriwa mwenye elimu ya Kidato cha Nne au cha Sita na astashahada katika

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Kuingiza taarifa za Wagonjwa katika Mifumo |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |

| | |
|---|---|
| **KAZI NA MAJUKUMU** | a) Kuendesha usahili kwa wahudumiwa (watu wenye ulemavu, wazee, familia zenye matatizo, watoto na washtakiwa).<br>b) Kutoa ushauri nasaha kwa wahudumiwa/ wateja.<br>c) Kufanya ukaguzi wa mazingira wanayoishi wahudumiwa ili kupata taarifa zao kamili.<br>d) Kupokea na kukusanya taarifa za ustawi wa jamii kutoka kwa wadau na vituo mbalimbali vya ustawi wa jamii.<br>e) Kuhoji na kuandaa taarifa za washtakiwa/ wateja.<br>f) Na majukumu mengine atakayopangiwa na Mkuu wake wa kazi. |

### 14.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 15.0 Dereva Daraja la II - (NAFASI 02)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini

**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 15.1 SIFA

Kuajiriwa wenye cheti cha kidato cha nne na leseni ya Daraja la C au C1 ya uendeshaji wa magari ambayo amefanyia kazi kwa muda usiopungua mwaka mmoja bila kusababisha ajali. Awe amehudhuria mafunzo ya msingi ya uendeshaji wa magari (basic driving course) yanatolewa na Chuo cha Mafunzo ya Ufundi Stadi (VETA) au chuo kingine kinachotambuliwa na Serikali. Waombaji wenye cheti cha majaribio ya Ufundi, watafikiriwa kwanza.

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Dereva |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | a) Kukagua gari kabla na baada ya safari ili kubaini hali ya usalama wa gari.<br>b) Kuwapeleka watumishi maeneo mbalimbali kwenye safari za kikazi.<br>c) Kufanya matengenezo madogo madogo ya gari.<br>d) Kukusanya na kusambaza nyaraka mbalimbali. |

| | |
|---|---|
| | e) Kujaza na kutunza taarifa za safari zote katika daftari la safari (Log book).<br>f) Kufanya usafi wa gari kila wakati.<br>g) Kufanya kazi nyingine kadri atakavyoelekezwa na msimamizi wake. |

### 15.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 16.0 Mpishi - (NAFASI 01)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini
**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 16.1 SIFA

Kuajiriwa mwenye elimu ya kidato cha nne na Astashahada/Stashahada ya fani ya upishi kutoka chuo kinachotambuliwa na Serikali.

| **KAZI** | Upishi |
|---|---|
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | a) Kufanya kazi zote za fani ya Upishi katika Hospitali<br>b) Kuandaa mahitaji ya chakula cha wagonjwa.<br>c) Kufanya usafi maeneo ya kuandalia chakula na vyombo.<br>d) Kuhudumia watumishi/wagonjwa kwa masuala ya chakula.<br>e) Na majukumu mengine atakayopangiwa na Mkuu wake wa kazi. |

### 16.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

## 17.0 Mtunza Bustani - (NAFASI 02)

**KITUO CHA KAZI**: Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini
**MASHARTI YA AJIRA:** Kujitolea, Mkataba wa Mwaka 1

### 17.1 SIFA

Kuajiriwa wenye elimu ya darasa la saba / kidato cha nne na uzoefu wa kutunza mazingira na bustani zaidi ya miaka miwili katika Hospitali.

| | |
|---|---|
| **KAZI** | Kutunza bustani |
| **MWAJIRI** | Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini |
| **MUDA WA MAOMBI** | 26/06/2026 – 03/07/2026 |
| **KAZI NA MAJUKUMU** | a) Kuandaa kitalu cha maua.<br>b) Kufanya usafi maeneo ya bustani pamoja na kumwagilia maua<br>c) Na majukumu mengine atakayopangiwa na Mkuu wake wa kazi. |

### 17.2 MSHAHARA NA POSHO

Malipo ya mshahara na posho yatazingatia **Mwongozo wa kujitolea katika utumishi wa Umma toleo la mwezi Juni, 2025.** Aidha posho nyingine zitalipwa kwa kuzingatia Sheria, Kanuni na Taratibu za Utumishi wa Umma.

### 18.0 MASHARTI YA JUMLA KWA WAOMBAJI WOTE

I. Waombaji wote wawe raia wa Tanzania wenye umri usiopungua miaka **18** na usiozidi miaka **35**.

II. Waombaji wawasilishe barua ya maombi na nakala zifuatazo: -
- Wasifu binafsi (CV).
- Cheti cha kuzaliwa.
- Kitambulisho cha Taifa (NIDA).
- Vyeti vya Elimu ya Sekondari **vilivyo thibitishwa kisheria.**
- Vyeti vya Utaalam katika fani husika.
- Usajili (Full Registration) na Leseni hai kwa kada husika.
- Muombaji aambatanishe picha ndogo (Passport size) mbili (2) na barua ya uthibitisho toka kwa Mtendaji wa Mtaa au Kijiji anacho toka kwenye barua ya maombi.

III. Awe Mmiliki halali wa vyeti vya kitaaluma;

IV. Awe na wadhamini **wawili** ambao ni watumishi wa Umma;

V. Awe hajawahi kuajiriwa katika Taasisi yoyote ya Umma tangu alipohitimu masomo.

VI. Vyeti vilivyotolewa na Bodi ya mitihani za nje ya Tanzania vya elimu ya kidato cha nne (CSE) au elimu ya kidato cha sita (ACSE) vinapaswa kuthibitishwa na Baraza la Mitihani (NECTA).

**19.0 JINSI YA KUWASILISHA MAOMBI**

Maombi yawasilishwe kufikia au kabla ya tarehe **03.07.2026** saa tisa na nusu alasiri (15:30HRS), kwa njia moja kati zifuatazo: -

i. Mtandao kwa barua pepe ps@szrh.go.tz
ii. Kwa mkono ifike katika Ofisi ya Masijala ya Wazi Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini (*Hakikisha unasaini katika kitabu baada ya kukabidhi*).
iii. Kwa Posta kupitia Anuani ifuatayo: -

**Mkurugenzi Mtendaji,**

**Hospitali ya Rufaa Kanda ya Kusini,**

**S.L.P. 272,**

**MTWARA.**

**Limetolewa na,**

MKURUGENZI WA HOSPITALI YA RUFAA KANDA YA KUSINI
26 JUN 2026
S. L. P. 272
MTWARA

Dkt. Herbert G. Masigati

**MKURUGENZI MTENDAJI**

**HOSPITALI YA RUFAA KANDA YA KUSINI**

**MTWARA**